NELKEN SCHOOL,
MALINDI-FUNGUNI,
P. O. Box 3992, Zanzibar.
Simu : 0773639363/0655058290.
Email: nelkenschool@gmail.com

Fomu Na……….

Picha ya mwanafunzi

# KANUNI NA UTARATIBU WA KUISHI BWENINI

**Ndugu, Mzee wa Mwanafunzi………………………………………………………………..**

**Utangulizi**

Kwa niaba ya Bodi ya skuli, waalimu, wafanyakazi na wanafunzi wa skuli ya Nelken tunampongeza mwanafunzi huyu kwa kuchaguliwa kujiunga na bweni katika skuli hii bora ya Nelken. Tunamkaribisha hapa skuli kwa moyo wa imani na kindugu.

Kanuni na taratibu zifuatazo zimewekwa kwa nia njema ili kufanya bweni kuwa ni mahali sahihi na salama kuishi ili kumuwezesha kila mmoja kufikia malengo sahihi yaliyowekwa.

**1. MAHITAJI MUHIMU.**

**a. Vifaa vinavyohitajika.**

i. **Sare za kuvaliwa bwenini (jozi 2).**

ii. **Wavulana**: Fulana rangi ya njano au buluu/bahari na suruali nyeusi ya kitambaa au khaki ya kawaida. Mavazi yasiwe na maandishi yeyote wala urembo. Kanzu na kofia.
**Wasichana**: Dera rangi ya njano/ buluu/bahari na suruali nyeusi ya kitambaa. Shungi ndefu rangi nyeupe isiwe na urembo. Kanga mivao miwili (doti mbili (2).
**NB**: Mavazi aina ya jinzi (Jeans), vimodo na yote yasiyo na heshima hayaruhusiwi kwa mwanafunzi.

iii. Godoro la futi (3 x 6), mto wa kulalia na Shuka 2 za rangi ya buluu au bahar au nyeupe, zisizo na marembo.

iv. **Mahitaji ya bafuni**: Ndoo/beseni, taulo, mswaki, dawa ya meno, sabuni, mafuta, ndala, kitana/shanuo,

v. **Mahitaji ya mezani**: Sahani, bakuli, kikombe. (Inashauriwa visiwe vya plastiki au vya kauri/kigae).

vi. **Mahitaji ya darasani**: vitabu vya masomo yote, madaftari, kalamu, rula, mkebe wa hesabu.

vii. **Karatasi nyeupe** saizi ya A4 Rim moja (zisizo na mistari).

viii. **Sanduku** moja au begi imara lenye kufuli la kuhifadhia vifaa vya mwanafunzi.

ix. **Msahafu 1** (Quran) kwa ajili ya madrasa.

x. Kiasi kidogo cha Fedha za matumizi (pocket money).

**b. Vifaa visivoruhusiwa kwa mwanafunzi wa skuli hii kuwa navyo:**

i. Vifaa vyote vya mawasiliano ya kielektroniki (Simu, tablet, laptop n.k). Hata ikiwa mbovu au imezimwa. Kifaa kitachokamatwa kitataifishwa moja kwa moja. Na adhabu nyingine kwa mwanafunzi itafuata.

ii. Vitafunwa kama bazooka (BG), peremende, ubani n.k.

iii. Machapisho, ala au rekodi (sauti, picha) za kuhamasisha mambo machafu yenye uhusiano na muziki, ulevi na mambo ya uasherati.
iv. Vifaa vyenye ncha kali. Mfano kisu, kiwembe, sindano, rula za chuma n.k
v. Viwashio na moto, kama vile kiberiti, Mshumaa, Sigara, Kandili, Jiko la tambi, n.k
vi. Vifaa vinavyotumia umeme kama pasi, blenda, chaja, hita, draya nk.
vii. Makopo/chupa za kupulizia gesi (aerosols), kama Dawa za mbu, Perfyum, rangi za kucha, piko, nk. Haviruhusiwi vipodozi vya aina yeyote, vito vya thamani na vifaa vya urembo. Spray inaruhusiwa.
viii. Kalamu za kujaza wino (refills) kama Fountain, Parker, Faber nk.
ix. Michezo ya bahati nasibu (puzzle game) na Kadi za karata nk.
x. Kiasi kikubwa cha fedha kinachozidi matumizi yake ya mwezi.
xi. Silaha ya aina yeyote.
xii. Wanyama wa kufugwa kama Paka, Mbwa, nk.
xiii. Biashara ya aina yeyote.

## 2. NIDHAMU

**Mwanafunzi wa skuli hii:**

i. Ni laazima avae sare wakati wote awapo ndani ya skuli na nje ya skuli kwa shughuli za skuli.
ii. Ni lazima kijana atoe taarifa kwa ngazi husika juu ya tatizo lolote linalomkwaza katika masomo yake.
iii. Ni lazima atunze usafi wake binafsi (wa mwili, mavazi, na malazi) na usafi wa mazingira. Usafi maalum utafanyika siku ya Jumapili. Nguo zilizoanikwa hairuhusiwi zilale kwenye kamba. Mwisho wa kuanua nguo ni saa 12.00 jioni. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu wala kunyoa kipara. Nywele za wavulana ziwe fupi daima, zipunguzwe kwa mkato wa kawaida.
iv. Lugha ya mawasiliano skuli ni **KINGEREZA pekee** isipokuwa wakati wa Masomo ya Kiswahili, Elimu ya Dini ya Kiislamu na Kiarabu**. Mawasiliano baina ya wanafunzi yawe kwa sauti ya chini na utulivu wakati wote.**
v. Ni lazima azingatie masomo yake na kukamilisha kazi anazopangiwa na walimu/wasimamizi wake.
vi. Kutunza mali yake binafsi na mali ya skuli. Pakitokea uharibifu wa makusudi wa mali ya skuli mhusika atafidia gharama za marekebisho au kununua kifaa kipya. Mharibifu asipopatikana, wanafunzi wote watawajibika kulipa fidia ya uharibifu huo. Skuli haitohusika na fidia ya upotevu wa mali ya mwanafunzi.
vii. Ni lazima ajiepushe na tabia zote mbaya zinazoweza kupelekea yeye kushitakiwa na kuadhibiwa ikiwemo uchafu, utoro, migomo, wizi, matusi, uasherati, ulevi, ugomvi, jinai nk.
viii. Ni lazima ashiriki kikamilifu ibada maalum kwa wakati wake ikiwemo swala za faradhi, swaumu nk.
ix. Ni marufuku kutoka nje ya eneo la skuli bila **ruhusa ya maandishi** kutoka kwa Mkuu wa skuli .
x. Hairuhusiwi kufanya vikao vya siri isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwalimu mkuu.
xi. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda kwenye majumba ya starehe, miziki na anasa nyingine.
xii. Kuchunga mipaka ya maeneo yaliyotengwa **maalum** kwa wavulana na wasichana wawapo skuli. Hairuhusiwi kuwasiliana kwa njia yeyote baina ya mvulana na msichana wa bweni. Itapobainika mvulana na msichana wamekaa pamoja peke yao **(hata darasani)** kwa sababu yeyote ile bila kuwepo mwalimu, ni kosa kubwa na watastahiki adhabu ya **kufukuzwa skuli mara moja**. Ripoti itapelekwa kwa wazee wao baadae.

3. **VYAKULA**
Skuli inaandaa vyakula vya kawaida viavyopatikana kwenye mazingira yetu. Ratiba ya chakula kwa wiki imeambatanishwa. Skuli haitoi vyakula maalum (special diet) vilivyo nje ya uwezo wake, hivyo palipo na mahitaji maalum mwanafunzi atajigharamia kwa ruhusa maalum. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula kutoka nje ya skuli.

4. **DHARURA NA MATIBABU**
Mwanafunzi atalazimika kupimwa afya na daktari anaetambulika na ripoti ya daktari iambatanishwe na fomu za kujiunga na skuli. Skuli itatoa huduma ya kwanza tu kwa mwanafunzi aliyepata dharura awapo skuli au bwenini kisha mwanafunzi atafikishwa hospitali kwa hatua Zaidi na mzazi/mlezi wa mwanafunzi ataarifiwa. Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kuhudhuria masomo kama mwanafunzi wa kutwa "Day Scholar" kwa sababu za ugonjwa wake. Bali atabakia nyumbani hadi atapopona kabisa na kurejea bwenini.

5. **WAGENI NA UJUMBE**
Ni marufuku kwa mwanafunzi kupokea wageni au ujumbe binafsi hata kama ni wa wazee wake/ndugu zake khalisa bila ruhusa kutoka kwa mkuu wa skuli. Siku maalum ya kutembelea wanafunzi wa bweni (Visiting Day) ni **Jumapili ya mwisho wa mwezi, kuanzia saa 9 alasiri hadi saa 12 jioni.** Wageni wanaokaribishwa ni wale tu wanaotambuliwa na skuli tu. Watatakiwa wafike kwanza ofisi ya Mwalimu Mkuu kwa utambulisho na kusaini kitabu maalum kabla ya kuonana na mwanafunzi.

6. **RUHUSA**
Ruhusa kwa dharura maalum tu, kama msiba, matibabu, au kutoa ushahidi mahkamani nk. itaombwa na mzee wa mwanafunzi na ruhusa kwa Mwalimu Mkuu au Mkurugenzi tu. Ruhusa hii ikitolewa, Mzazi/mlezi ni lazima afike yeye mwenyewe au mwakilishi wake **anayetambulika skuli** ili kumchukua mtoto na baadae kumrejesha baada ya dharura kuisha. Ikibainika kuwa dharura iliyotolewa haikuwa sahihi, bali ni kisingizio tu ili mtoto arudi nyumbani, mtoto atafukuzwa **SKULI** moja kwa moja.

7. **HAKI YA MWANAFUNZI.**
Mwanafunzi anastahiki kupewa elimu sahihi, chakula bora, na malazi mazuri kwa kufuatana na utaratibu wa skuli. Pia anastahiki mwanafunzi kulindwa, kuheshimiwa, kuthaminiwa utu wake, kusikilizwa maoni yake, kujitetea kufuatia tuhuma yeyote dhidi yake na kukata rufaa katika ngazi za skuli kufuatia adhabu isiyoridhisha. Kwa upande wake ana haki ya kutumia vyema fursa hii katika kujielimisha akitambua kuwa kuwepo kwake bwenini ni bahati tu hivyo ana deni kwa wazazi na jamii.

8. **MAMLAKA YA SKULI**
Mkuu wa Skuli anayo mamlaka kamili kusimamia maisha ya mtoto wa Bwenini. Ikiwa iko haja anaweza kuingia bwenini au kumruhusu mwingine yeyote kuingia bwenini kwa kushirikiana na matron na patron wakati wowote kwa sababu maalum ikiwemo: ukaguzi wa usafi, kubadili au kuripeya samani, kumhudumia mgonjwa, na kusimamia nidhamu kwa mujibu wa kanuni zilizomo humu.

**9. ADHABU**

Mwanafunzi atakaekiuka kanuni za nidhamu kwa mara ya kwanza ataonywa kwa mdomo na kamati za nidhamu. Akirejea kosa ataonywa kwa maandishi. Asipojirekebisha atafukuzwa skuli. Iwapo mwanafunzi atafukuzwa skuli kufuatia utovu wa nidhamu fedha iliyolipwa skuli haitarejeshwa.

**10. HITIMISHO**

Tunashukuruni wazazi/walezi wote kwa namna ya kipekee kwa ushirikiano wenu na kuendelea kutuamini. Tunaahidi kuzidi kutumia taaluma zetu vyema, uzoefu, na ari tuliyonayo katika malezi bora ya kijana wetu kwa manufaa ya taifa, dunia na akhera yake.

***Nambari za mawasiliano: 0773193232 (Mkuu wa skuli); 0655058290 (ofisini).***

**NELKEN SCHOOL**

**P. O. BOX 3992, MALINDI- ZANZIBAR.**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA BWENI MWAKA 2023.**

*(Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi pamoja na Mwanafunzi na ithibitishwe na Sheha wa shehiya anayoishi Mwanafunzi*)

**Sehemu A: ijazwe na Mwanafunzi**

Mimi …………………………………………………………………………………… (Jina la mwanafunzi)

Nimezisoma na kuzielewa kanuni hizi na taratibu za skuli ya NELKEN SCHOOL. Kwa kuweka saini yangu hapa chini nakubali kwa khiyari yangu, nitaitumia vyema nafasi niliyopewa ya kuishi bwenini katika skuli hii iliyoko Malindi- Zanzibar, kuanzia tarehe 02/03/2023 hadi 10/11/2023. Nitakuwa tayari kufuata kanuni na taratibu zote za skuli kwa ujumla wake wakati wote niwapo skulini. Natambua kuwa kuzikiuka taratibu hizo kwa makusudi, hatua zinazostahili za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa dhidi yangu ikiwemo kusimamishwa masomo au kushitakiwa kwa mujibu wa sheria.

…………………………………… (Saini ya Mwanafunzi) ……………………….Tarehe………………………………

**Sehemu B: ijazwe na Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.**

Mimi ……………………………………………………. (Jina la Mzazi/Mlezi) wa ……………………………………………………..

Kwa kuweka saini yangu hapa chini nakubali kwa ridhaa yangu, nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo skulini analazimika kufuata kanuni na taratibu skuli na kuwa mtiifu kwa walezi wake. Pia nakubali kulipa ada na michango kwa wakati na maelekezo mengine yatakayotolewa skulini. Nitatoa ushirikiano kwa kadri ya uwezo wangu pindi itapohitajika ili kufikia lengo lililokusudiwa.

…………........(Saini ya Mzazi/Mlezi) Namba ya simu.................................. Tarehe…………

Sehemu C: ijazwe na **SHEHA wa shehiya anakoishi mwanafunzi**:

Mimi……………………………………………………………… (jina la Sheha) ambaye ni Sheha wa Shehiya ya …………………… Ninathibitisha na kumtambua ndugu.............................................................kuwa ni Mzazi/Mlezi wa kijana mtajwa hapo juu aliyechaguliwa kujiunga na bweni katika skuli ya NELKEN iliyoko MALINDI, Unguja. Nathibitisha kuwa kijana huyu ana tabia njema na anastahili kupewa nafasi hiyo.

……………………(Saini ya sheha); Nambari ya simu……………………………………..Tarehe……………

Mhuri wa sheha……………………………

**NELKEN SCHOOL.**
**P. O. BOX 3992, MALINDI- ZANZIBAR.**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.

REF: NO. NS/MEX/VOL.II/2022. DATE:…………………

TO THE MEDICAL OFFICER,
………………………………………… HOSPITAL,
P. O. BOX. ………………………………………….
MOBILE: ………………………………………….

**REF. STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

**…………………………………………………………** (Name of the student)

Please Dr, kindly examine the above-named student who has been selected to join this school for his/her fitness as a boarding student in the following (To be completed by a medical officer)

1. Eyesight………………………………………
2. Hearing………………………………………..
3. Limbs……………………………………………..
4. SPECIMEN:
   i. Stool………………………………………
   ii. Urinalysis……………………………………
   iii. Blood count ……………………………………
   iv. Neurosis…………………………………
5. Asthma…………………………………………
6. Tuberculosis…………………………………..
7. Pregnancy……………………………………
8. Other serious diseases: -
   i. Venereal disease…………………….
   ii. Leprosy…………………………………
   iii. Epilepsy…………………………………
   iv. Ulcers…………………………………..
   v. Bilharzias………………………………
   vi. Mental illness……………………....
   vii. Diabetes…………………………………
   viii. Heart diseases………………………..
   ix. Sickle cell anemia…………………….
   x. Nosebleeds……………………………..
   xi. Urinary incontinence………………
   xii. Measles ………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**: (To be completed by a Medical Officer)
I have examined the above and consider him/her to be physically **FIT /UNFIT** as a boarding student.

Date: …………………………… Signature: …………………………… (and official stamp)
Working Station: …………………………… Designation: ……………………….

---

NB: May you please return this form back to the school in a sealed envelope.

| SEHEMU HII NI KWA MATUMIZI YA OFISI TU | |
|---|---|
| MALIPO YA ADA KABLA YA KUANZA MASOMO | |
| MALIPO | NAMBARI YA RISITI |
| KIINGILIO: | |
| MASOMO: | |
| BWENI: | |
| MENGINEYO: | |
| **JUMLA**: | |
| MATOKEO YA USAILI (INTERVIEW): | Amepata wastani wa alama ………..Daraja ……... |
| KIJANA **AMEKUBALIWA / HAKUKUBALIWA** KUJIUNGA NA SKULI | |
| NAMBARI YA KUANDIKISHWA: | |

Tunamtakia kijana wetu mafanikio mema.

…………………………………………..

MKUU WA SKULI

NELKEN, MALINDI